JINA............................................NAMBARI......................DARASA........

102
MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA
KISWAHILI
KIDATO CHA TATU
MACHI/ APRILI 2019

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA
HATI YA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI
KISWAHILI
MUDA 2 ½

## MAAGIZO

(i) Jibu maswali yoye.
(ii) Majibu yotte yaandikwe katika nafasi ulizotengewa baada ya kila swali
(iii) Lazima maswali yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
(iv) Hakikisha umejibu maswali yote.

**Kwa matumizi ya mtahini.**

| SEHEMU | | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|---|
| 1 | MUHTASARI | 15 | |
| 2 | SARUFI NA LUGHA | 35 | |
| 3 | ISIMUJAMII | 10 | |
| 4 | FASIHI SIMULIZI | 20 | |
| | JUMLA | 80 | |

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

**UFUPISHO: (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Ukekeketaji ni mfumo wa upasuaji unaofanyiwa wanawake na wasichana sehemu ny duniani. Istilahi hii ya ukeketaji ina maana pana kwani inaweza kutumiwa kuelezea upa tohara kwa wasichana na ukataji wa sehemu za siri kwa wanawake.

Ukeketaji haupatikani tu katika bara la Afrika bali katika sehemu nyingi ulimwengu Umri ambapo ukeketaji hufanyika hutegemea jamii inayohusika. Mwanamke anaweza kufanyiwa ukeketaji siku chache baada ya kuzaliwa au baada ya kujifungua mtoto wake kwanza. Miongoni mwa jamii ambazo hupasha tohara wanawake, huthamini sana amal kwani kwao ni hatua muhimu ya mpito wa maisha katika jamii za jadi mwanamke hupitishwa kutoka rika moja hadi lingine, yaani kutoka utotoni na kuingia kwenye utu u

Ukeketaji unafungamana na sherehe ya kuwapa wasichana mafunzo kuhusu kanuni uzazi, malezi na ndoa. Dhima kuu ya sherehe hiyo ya kuwapasha wasichana tohara ina ya kwamba ni kuwapunguzia wanawake uchu na kuhifadhi ubirika. Jamii nyingine hetekeleza tohara kwa sababu za kidini zinazoshikilia kuwa mwanamke aliyetahiriwa h nadhifu. Wengine wanaamini kuwa tohara hufanya watoto wanapozaliwa kuwa na nafa nzuri ya kuishi, ilhali wengine hupashwa tohara ili wapate waume wa kuwaoa. Kweny jamii ambazo wanaume wanasisitiza tohara kama wa kigezo cha mwanamke kuolewa ukeketaji umeshamiri. Katika jamii kama hizi wanaume huwa hawataki kuoa wanawak ambao hawajatahiriwa.

Wanawake wenyewe huhakikisha ya kwamba watoto au wajukuu wao wanapelekw kupashwa tohara. Wakati mwingine mipango ya siri hupangwa na kina mama hao pam mangariba, kuhakikisha kuwa jambo hili linatekelezwa. Kwa hivyo jambo hili la ukek lina utata miongoni mwa jamii nyingi ulimwenguni.

Hata hivyo ukweli ni kwamba swala zima la ukeketaji lina madhara makubwa na linamdhalilisha mwanamke. Katika hali ya upashaji tohara wanawake huvuja damu ny na aghalabu huaga dunia. Wale wanaopona huwa kwenye hatari ya kuambukizwa mar ya zinaa ambayo huharibu sehemu za uzazi. Kwani madaktari wanadai uchungu wa uz huwa mwingi na hudumu muda mrefu.

Kwa sababu tohara hufanywa mara moja kwa mwaka, wasichana wote wa rika moj hukusanyika mahali maalum ili kufanyiwa tohara. Kifaa ambacho hutumiwa sana ni wembe. Wembe huo hutumiwa kuwakatia wasichana wote ambao wanapashwa tohara kipindi hicho. Wembe huo hauchemshwi angalau kuua viini vinavyosababisha na kue magonjwa mbalimbali. Hali hii huwaweka wasichana hao kwenye hatari ya kuambuki ugonjwa hatari wa ukimwi. Licha ya hayo wasichana waliotahiriwa nguvu za kinga dl magonjwa hupungua. Kwa hivyo wanaweza kupata magonjwa mengine ya kuambuki urahisi. Kwa hivyo ukeketaji ni tendo la hatari na la kumdhalilisha mwanadamu amba linastahili kulaaniwa.

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Ukizingatia mambo muhimu anayoeleza mwandishi, fupisha aya tatu za kwanza (maneno 70). (alama9)

Matayarisho

Jibu

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

(b) Fupisha ujumbe wa mwandishi katika aya mbili za mwisho (maneno 50). (alama6)

Matayarisho

Jibu

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

**SARUFI NA LUGHA (ALAMA35)**

(a) Toa mifano miwili ya : (alama2)

(i) Sauti ghuna ambazo ni vipasuo

(ii) Sauti si ghuna ambazo ni vikwamizo

(b) Onyesha silabi kisha ueleze muundo wazo katika neno: (alama4)
Chura

(c) Weka shadda katika sentensi ifuatayo. (alama1)
Tunda li mezani

(d) Tunga sentensi ya neno moja yenye viungo vifuatavyo: (alama3)
(i) Kikanushi

(ii) Wakati ujao

(iii) Kitendwa

(iv) Mzizi wa kitenzi cha silabi moja

(v) Kauli (tendea)

(vi) Kauli (tenda)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

(e) Ainisha vielezi katika sentensi ifuatayo. (alama2)
Nguvumo aliimba taarabu vizuri jana.

(f) Onyesha viwakiloshi katika sentensi zifuatazo kisha ueleze ni vya aina gani. (alama2)
(i) Sisi wenyewe tutapika chajio.

(ii) Wengine hawapendi kusoma riwaya.

(g) Eleza miundo yoyote miwili ya nomono katika ngeli ya U – zi. (alama2)

(h) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu. (alama2)
Yeye huwasili kwao nyumbani saa tatu jioni.

(i) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili tofauti ya kistari kirefu. (alama2)

(j) Andika katika usemi wa taarifa. (alama3)
"Mwalimu, nitahitajika kuwa nyumbani kwetu kesho jiono." Umulkheri alisema.

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

(k) Unda nomino mbili kutokana na vitenzi vifuatavyo. (alama2)
(i) Linda

(ii) Laani

(l) Tunga sentensi mbili ukitumia kiambishi 'ni' kama kitenzi na kama kielezi. (alama2

(m) Tambua matumizi ya kiambishi 'po' katika sentensi ifuatayo. (alama2
Mwanafunzi alipofika, alienda alipo mwalimu.

(n) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo. (alama2
Mtoto msichana alicheka kwa furaha.

(o) (i) Sentensi changamao ni nini? (alama

(iii) Tunga sentensi moja changamano. (alama1)

(p) Yakinisha sentensi ifuatayo. (alama2)
Usingekuwa na nia safi, asingekusamehe

(q) Andika katika hali ya wastani. (alama2)
Jipake hilo lilirarua guo lake.

(r) Andika kwa umoja. (alama1)
Pulikeni wanetu, msicheze na dunia.

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

**ISIMU JAMII (ALAMA10)**

(a) Fafanua maana ya: (alama3)

(i) Lafudhi

(ii) Lahaja

(iii) Krioli

(b) Eleza sababu zinazofanya mazungumzo yanayotokea katika mazingira mbalimbali kuw… tofauti za kimatumizi ya lugha. (alam…

**USHAIRI ANDISHI (ALAMA 20)**
**Jibu swali la 6 au 7**
**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Kazi ni kazi
Kazi inozaa mazo
Kazi ni uhai
Kazi hukuza uchumi.

Kazi haiwi kazi
Kazi paso uhai
Kazi msingi wa maisha
Kazi huleta maendeleo.

Kazi ni Baraka
Uhai ni Baraka
Uhai ni kazi
Kazi asofanya
Baraka akosa
Na uhai vilevile.

Kokoiko! Kucha kuchele
Kengele ngelengele

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

Kiumbe wamaka
Kumeekucha!kazi kihofia
Kusudi blanketi tavuta
Kujigubika gubigubi
Kujisingizia ndwele.

Kazi mzembe hutamani
Ni damuyo kuilaza
Na kuupiga uvivu.

Kazi kutotamani fahamu
Ni kutamani mauti
Na mauti yakikufika
Ole mbwako tajijutia!

**Maswali**

(a) Eleza kichwa mwafaka cha shairi hili (alama2)

(b) Taja na ueleze dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (alama2)

(c) Fafanua sifa **mbili** za mashairi huru zinazojitokeza katika shairi hili. (alama2)

(d) Eleza mbinu **mbili** za uhuru wa mshairi zinazodhihirika katika shairi hili (alama4)

(e) Mshairi anasema nini katika ubeti wa mwisho? (alama3)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

(f) Taja na ueleze fani tatu za kifasihi zilizotumika katika ubeti wanne. (alama3)

(g) Eleza toni inayojitokeza katika shairi hili. (alama2)

(h) Andika visawe vya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama2)
(i) Ndwele

(iii) Uvivu

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

**FASIHI SIMULIZI (ALAMA20)**
**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Vijana wawili walifanya mazoea ya kuchelewa shuleni kwa kwenda kucheza michezo ya kompyuta katika kituo Fulani karibu na kwao. Mwalimu wao aliamua kichunguza kwa hakika kilichokuwa kinawachelewesha wanafunzi wake.

Siku moja walifika chuoni wakiwa wameandaa kisa cha uwongo, kama ilivyokuwa mazoea yao. Walipompa sababu zao, kama kawaida , mwalimu alitabasamu na kuwaambia. I neno, ninaelewa kuwa baiskeli ilipata panchari. Vujana walitazamana kwa furaha wakijua kwamba kwa mara nyingine wamefaulu kumchezea mwalimu, lakini hawakujua kuwa mwalimu naye kawaandalia mtihaniwake. Aliwapa karatsi iliyokuwa na swali moja tu na kuwaweka katika vyumba tofauti.

Eleza kwa kifupi ni gurudumu gani lililopata pancha – la mbele au la nyuma, swa lilisoma. Kwa maana katika ujanja wao hakukumbuka kuafikiana juu ya jambo rahisi ka mmoja aliandika la mbele..na mwingine la nyuma. Si viboko hivyo walivyopata…..

**Maswali**

(a) Tambua utunzi na kipera kinachowasilishwa na kifungu hiki (alam

(b) Fafanua sifa za kipera hiki (alam

(c) Eleza umuhimu wa kipera hiki (alam

(d) Taja miktadha ambamo ulumbi hutumika katika jamii (alam

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com